



THE
LUTHERAN
WORLD
FEDERATION

Office of the
General Secretary

lutheranworld.org

Geneva, 11.03.2020

Ndugu zangu wapendwa,

Kila siku tunapokea habari mpya kuhusu kuenea kwa COVID-19, virusi vyा Corona. Nchi ny ingi zimechukua hatua za udhibiti ili kuzuia kusambaa kwa virusi hivyo na pia kulemewa kwa mifumo ya huduma za afya.

Tunasoma katika "watchword" (Utaratibu wa kujisomea Neno la Mungu wa Moravian) Jumanne tarehe 10 mwezi wa 3:

Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na moyo wa kiasi. (2Timoteo 1:7).

Tunataka kuyatia moyo makanisa wanachama wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), viongozi wake, na washarika wa makanisa hayo kuweka mstari huu moyoni katika nyakati hizi zenyе changamoto.

Huu ni wakati wa kuendelea kuamini uwepo wa huruma za Mungu katika maisha ya mwanadamu. Tunao ujasiri tukijua kuwa Mungu hatuachi kamwe, hata kama itamaanisha kupitia mateso ya msalaba. Tunauona msalaba wa Yesu Kristo kama alama ya nguvu na tumaini letu.

Wito wa kuwa na nidhamu binafsi uliotajwa katika mstari wa Biblia hapo juu, unalinganishwa na wito wa kumpenda jirani. Upendo na nidhamu binafsi vinawekwa katika safu moja, hasa katika siku hizi. Kwa kujizuia kukutana au kujumuika kusiko kwa lazima, tunaweza kuonesha upendo wetu na kujali wale walio katika hatari zaidi ya kuambukizwa virusi hivi. Tunawasihi mdumishe nidhamu binafsi kama zawadi ya Mungu.

Katika hali ya pekee, hii inaweza kuhitaji kufikiri tena juu ya tamaduni za mikusanyiko na ibada. Tunalishukuru kanisa la Asia ambalo ni mwanachama wa FKMD kwa kutoa mwoongozo katika hili (<https://www.lutheranworld.org/news/churches-asia-advise-prudence-covid19-outbreak>) na kuwatia moyo ninyi kuchukua hatua zinazostahili kwa lengo la kuzuia virusi kuenea zaidi na kuwalinda wale walio katika hatari zaidi.

Tunaendelea kuwashauri kufuata maelekezo ya idara za afya ya jamii katika nchi zenu. Habari ny ingi za uongo zinasambaa. Zuieni kuenea kwa habari zisizo sahihi kwa kufuatilia habari kutoka vyombo rasmi, ikiwa ni pamoja na Shirika la Afya Duniani (<https://www.who.int/emergencies/diseases/novel-coronavirus-2019>).

Tunaalika makanisa wanachama kuombeana hasa kwa nchi na makanisa ambayo yako katika kiini cha mlipuko wa virusi hivyo. Kuna ugumu inaposhindikana kuonesha mahusiano ya kawaida ya kila siku kama ilivyo kawaida. Wafanyakazi na wamiliki wa biashara wanahofia kuhusu mustakabali wao. Watu wa rika zote wanahofia juu ya afya zao.

Tunapokabiliana na changamoto hii, tunawasihi pia muwakumbuke hao wanaokumbana na changamoto nyingine za kiafya katika maisha yao ya kila siku: homa ya dengue, Malaria, VVU/UKIMWI ambavyo vimeendelea kuwa tishio na magonjwa mengine yanayohatarisha maisha.

Ni maombi yetu kuwa virusi vya Corona visitufanye kuwa watu wasiojali. Bali tuelewe kwa upya jinsi maisha ya mwanadamu yalivyo katika hatari. Huu uwe wakati wa kuwajibika kumuombea na kumuonesha upendo jirani (Luka 10:25-37).

Kwa unyenyekevu tunawashirikisha habari hizi za kutia moyo huku tukiendelea kuwaombea.

Wenu katika Kristo,



Askofu Mkuu Dkt Filibus Panti Musa
Rais wa FMKD



Mchg Dkt Martin Junge
Katibu Mkuu wa FMKD